JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

# TAARIFA YA HALI MBAYA YA HEWA KWA MWEZI JULAI NA AGOSTI, 2025

## 1.0 UTANGULIZI

Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Agosti, 2025 vipindi vya ukavu pamoja na baridi ya wastani hadi baridi kali hususan nyakati za usiku na asubuhi iliendelea kujitokeza katika maeneo mengi nchini. Hali hii ilisababisha upungufu wa unyevu ardhini, kupungua kwa maji na malisho pamoja na kuwepo kwa hali vumbi. Hata hivyo, vipindi vya upepo mkali uliofikia au kuzidi kasi ya kilomita 40 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo, hususan maeneo ya ukanda wa pwani na maziwa makuu.

Ingawa hali ya ukavu imeendelea kujitokeza katika maeneo mengi ya nchi lakini vipindi vichache vya mvua vilijitokeza katika maeneo ya ukanda pwani, Ziwa Victoria na maeneo yenye miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki. Aidha, hali ya hewa iliyojitokeza pamoja na athari zake imeendana na taarifa ya mwelekeo wa msimu wa Kipupwe (Juni-Agosti), 2025 iliyotolewa mwezi Mei 2025.

### 1.1 Mvua kubwa kwa mwezi Julai na Agosti, 2025

Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Agosti, 2025 vipindi vichache vya mvua vilijitokeza katika maeneo machache, hususan ukanda wa pwani, ziwa Victoria na maeneo yenye miinuko ya nyanda za juu Kaskazini mashariki. Katika kipindi hiki, mvua kubwa ya milimita 59.4 ndani ya saa 24 iliripotiwa Musoma, mkoani Mara mnamo tarehe 18 Agosti 2025. Mvua hii ilisababisha mafuriko katika mji wa Musoma na kupelekea majeruhi takribani watu 31(Angalia kielelezo 1).

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*728G _ 01/2023*



**Kielelezo 1:** Kikosi cha zima moto na uokozi kikiendelea na juhudi za uokozi katika mji wa Musoma (Chanzo: Mazingira FM).


### 1.2 Hali joto kwa mwezi Julai, 2025

Katika kipindi cha mwezi Julai 2025, hali ya joto iliendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchini nyakati za mchana, hata hivyo hakukuwa na viwango vya joto kali zaidi vilivyoripotiwa katika kipindi hiki. Aidha, vipindi vya baridi kali vilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi, hususan mikoa ya Mbeya na Njombe. Katika mwezi huu kituo cha Igeri (Mkoa wa Njombe) kiliripoti viwango vya nyuzi joto chini ya 10 °C kwa muda wa siku 31. Ikifuatiwa na vituo vya Uyole na Mbozi (mkoa wa Mbeya) kwa siku 29 na 19 mtawalia.

Jedwali 1. Idadi ya siku ambazo viwango vidogo vya joto la chini vilivyojitokeza mwezi Julai, 2025.

| Kanda | Kituo | Idadi ya siku (≤ 10 °C) | Kiwango cha chini zaidi kurekodiwa ($^0$C) |
|---|---|---|---|
| **Nyanda za juu kusini Magharibi** | Igeri | 31 | 5.4 °C |
| | Uyole | 29 | 6.0 °C |
| | Mbozi | 19 | 7.6 °C |
| | Sumbawanga | 11 | 8.3 °C |

Kielelezo 2 kinaonyesha viwango vya joto la chini vilishuka zaidi wiki ya nne ya mwezi, na kiwango cha chini zaidi cha joto cha nyuzi joto 5.4 °C kiliripotiwa katika kituo cha Igeri mnamo tarehe 31 Julai, 2025.




**Kielelzo 2.** Viwango vya joto la chini kituo cha Uyole na Igeri katika mwezi Julai, 2025.

### 1.3 Upepo Mkali kwa mwezi Julai, 2025

Katika kipindi cha mwezi Julai, 2025 vipindi vya upepo mkali unaofika na kuzidi kilomita 40 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, hususan maeneo ya ukanda wa pwani (Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Lindi, Mtwara na visiwa vya Unguja na Pemba), Songwe, Mpanda na Mahenge. Hali hii iliashiria kuendelea kwa msimu wa Kipupwe ambao hutawaliwa na upepo mkali wa kusi.


### 1.4 Hali joto kwa mwezi Agosti, 2025

Kwa kuzingatia hali ya hewa ya muda mrefu (Klimatolojia) kwa mwezi Agosti, hakuna hali ya joto kali iliyojitokeza katika kipindi hiki. Hata hivyo, viwango vidogo vya joto la chini viliendelea kujitokeza katika baadhi ya maeneo nchini, hususan nyanda za juu kusini magharibi. Kiwango kidogo zaidi cha joto la chini kilichorekodiwa katika kituo cha Igeri (mkoa wa Njombe) kilikuwa ni nyuzi joto 4.2 °C mnamo tarehe 5 Agosti, 2025. Aidha, katika kipindi hiki vituo vya Igeri na Uyole viliripoti viwango vya joto chini ya nyuzi joto 10 °C kwa siku 30 na 28 mtawalia. Jedwali namba 2 linaonyesha idadi ya siku ambazo kituo kimerekodi kiwango cha joto la chini cha nyuzi joto 10 °C au chini ya nyuzi joto 10 °C.

Jedwali 2. Viwango vidogo vya joto la chini vilivyojitokeza mwezi Agosti, 2023

| Kanda | Kituo | Idadi ya siku (≤ 10 °C) | Kiwango cha chini zaidi kurekodiwa ($^0$C) |
|---|---|---|---|
| **Southwestern highlands** | Igeri | 30 | 4.2 °C |
| | Uyole | 28 | 5.0 °C |
| | Mbozi | 23 | 6.2 °C |
| | Sumbawanga | 6 | 8.3 °C |

Kielelezo cha 3 kinaonesha viwango vya joto la chini kwa kila siku kwa mwezi Agosti, 2025 kwa vituo vya Uyole na Igeri. Kwa ujumla, hali ya baridi kali iliendelea kujitokeza katika wiki ya kwanza hususan Igeri. Hata hivyo, viwango vya joto la chini vilionyesha kupanda mwanzoni mwa wiki ya nne na kushuka tena kuelekea mwishoni mwa mwezi.




**Kielelzo 3.** Viwango vya joto la chini kituo cha Uyole na Igeri katika mwezi June, 2025.

### 1.5 Upepo Mkali kwa mwezi Agosti, 2025

Katika kipindi cha mwezi Agosti, 2025 vipindi vya upepo mkali unaofika kilomita 40 hadi 50 kwa saa vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini ikiwemo ukanda wa pwani (Mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Mtwara pamoja na Visiwa vya Unguja na Pemba), kati (Mikoa ya Singida na Dodoma) pamoja na maziwa makuu. Nguvu ya upepo mkali ilisababisha athari mbalimbali katika maeneo hayo ikiwemo kusambaa kwa vumbi, kupeperushwa kwa takataka, kupungua kwa uono na kuathiri ubora wa hewa. Maeneo ya mwambao wa pwani ya bahari yalipatwa na vipindi vya mawimbi makubwa na kuathiri baadhi ya shughuli zinazofanyika baharini sambamba na kuhatarisha jamii zinazofanya shughuli mbalimbali katika maeneo ya mwambao.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*728G _ 01/2023*

*Matukio haya ya hali mbaya ya hewa yanaonesha ongezeko la changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na umuhimu wa kutekeleza mikakati thabiti ya kukabiliana na mabadiliko hayo ili kulinda jamii na mazingira*.

*Imetolewa: tarehe 9 Septemba, 2025*
**Na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610

Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz